

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

**MKOA WA NJOMBE**

**Simu: 026-2968833**

**Faksi: 026- 298832**

**E- mail: [td@njombetc.go.tz](mailto:td@njombetc.go.tz)**

**[njombetc@gmail.com](mailto:njombetc@gmail.com)**

**Tovuti: [www.njombetc.go.tz](http://www.njombetc.go.tz)**



**S.L.P 577,  
NJOMBE.**

**05/10/2017**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU  
BEI ELEKEZI YA MBOLEA AINA YA DAP NA UREA.**

Katika kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikapo 2025, juhudi kubwa imefanyika ili kutimiza malengo ya kimkakati kuelekea kilimo cha kibiashara. Moja ya mikakati hiyo ni kuhakikisha mkulima anapata pembejeo za kilimo hususani mbegu bora, mbolea na viuatilifu.

Katika utekelezaji wa mkakati huo Serikali kupitia Mamlaka ya Mbolea Tanzania TFRA, ilikubaliana na mfumo wa uagizaji mbolea kwa pamoja kupitia makampuni ya mbolea na kuwa na bei elekezi kila Halmashauri kwa **Mbolea aina ya DAP ni Tsh. 53,007/ kwa mfuko wa kilogram 50** na **UREA ni Tsh.40,428 kwa mfuko wa Kilogram 50**. Bei hizi ni bei ambazo mkulima anatakiwa kununua kutoka kwa muuzaji na zitakuwa zikibadilika mara tu bei nyingine zitakapokuwa zimetolewa na Mamlaka husika.

Mkulima hakikisha mbolea utakayonunua unauziwa kwa bei hizi elekezi na unapewa risiti mara ununuapo mbolea hizi.

Muuzaji atakayekaidi maelekezo haya hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

***Imetolewa Na,  
Afisa Habari.  
Halmashauri ya Mji Njombe.***